Kuchaguliwa kwa Wachache na Miaka Elfu Moja

(The Rapture and Millennialism)

Na

Ellis P. Forsman

Kuchaguliwa kwa Wachache na Miaka Elfu Moja

(The Rapture and Millennialism)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

Kuchaguliwa kwa Wachache Na Miaka Elfu Moja

Math. 25: 31-46

Mmoja wa mwajiriwa mwenzangu wakati Fulani alizungumzia kuhusu kuchaguliwa kwa wachache na maajabu wakati itakapotokea.

Je neno hili linaleta maana kwako? Je haya ni mafundisho ya kibiblia? Hata ni neno la kibiblia? Kwa nini dini zote zimefurahi kuhusu neno hili "Kuchaguliwa wachache"? Je kile ambacho ulimwengu wa kidini wanafundisha kuhusu "Kuchaguliwa wachache" inakubaliana na mafundisho ya kibiblia?

Jaribio la kuchaguliwa kwa wachache inadhaniwa kwamba ni muda ambao Bwana atakuja kuwachukuwa watu wake katika dunia hii na kuwa safirisha katika kituo sehemu ambayo haijulikani ambapo watakaa kwa miaka saba.

Wenye haki waliokufa watafufuliwa kutoka katika wafu.

Alafu wenye haki wote wanaoishi watakutwa katika sehemu hii ya muda mfupi.

Watu wanaobaki duniani hawatajua walipopelekwa watakatifu wote. Hawataweza kuhesabu au kujua kutoweka kwao. Hawatakuwa na maelezo ya kutosha kuhusu makaburi yalioachwa wazi na miili iliyofufuliwa.

Kuchaguliwa Kwa Wachache Na Mihangaiko

Labda, hiki kikundi kilicho chaguliwa wako na Bwana wakati wa kuchaguliwa wachache, pia inadhaniwa kuwa kutakuwa na kuhangaika katika dunia.

- Kutakuwa na uoga.
- Kutakuwa na maajabu.
- Kutakuwa na vifo vingi.

Labda, hakuna mtu atakayejua kinachoendelea, bali wote watakubali kwamba dhambi kama hii haijawahi kutokea kabla.

Wakati wa 1970, sinema ya kidini inaonyesha kuhusu kuchaguliwa kwa wachache ilitazamwa na wengi. Mimi binafsi sijawahi kuiangalia sinema hii, lakini nimewahi kusikia.

Waonyeshaji waliahidi watazamaji kwamba hawatakuwa kama walivyo baada ya kuiangalia sinema hii. Uongo na dhana potofu ndiyo imejaa katika picha hii. Mipango ya sinema hii imejengwa katika runinga ambayo labda itatokea baada ya kikundi hiki kuchaguliwa. Imeegemea katika kichwa cha habari kutoka katika magazeti kuhusu kupotea kwa mamilioni ya watu bila maelezo ya watakapofikia.

Kuna dhambi mbaya katika skeli ya dunia. Kifo cha kikundi kikubwa cha watu inahabarishwa kutoka katika vianzo vyote vya dunia. Kila mmoja katika dunia atajazwa uoga, na mwigizaji huyu amenyamaza na kukusanywa kana kwamba alikuwa anatoa viwango katika soko la kubadisha fedha.

Watu wengi wanahojiwa katika jitihada za kuelewa kinachoendelea. Rais wa Marekani ni mmoja kati ya waliopotea.

Kijana mmoja katika "Onyesho la usiku wa leo" amepotea alipokuwa anaimba wimbo wa dini mbele ya watazamaji wengi. Wapiga picha wametazamwa wakiwa wamechukizwa na mshangao mkubwa kwa kile kilichotokea.

Sinema inaisha na hatimaye kupata wazo kwamba wachache wamechukuliwa.

Je Biblia inafundisha kwamba kikundi cha wachache ndiyo watakao chukuliwa? Hakika hakuna! Jaribio hili la uongo linapingana na mafundisho ya Biblia.

Niruhusu nidokeze baadhi ya mafundisho ambayo si ya kibiblia katika somo hili.

Uwazi katika Nadharia

Kwanza kabla ya yote, kuchaguliwa huku inaeleza ziara nyingi, au kutokea kwa Yesu Kristo.

Nadharia hii ya uongo inabashiri kuja kwa Yesu kwa ajili ya watakatifu mwanzo wa kuchukuliwa kwa kikundi hiki.

Alafu baadaye Yesu anakuja na watakatifu mwisho wa kuchukuliwa kwa hawa wachache, baada ya kila mmoja katika dunia kumwua mwenzake katika vita kuu iitwayo Armageddon kwanzia miaka 1000 uongozi utakaokaa katika kiti cha Daudi Yerusalemu baada ya kumjengea Solomoni hekalu kubwa.

Hiyo inamanisha kwamba kulikuwa na kuja kwa Yesu mara mbili kati ya miaka michache, ambayo hasa, inapingana na fundisho la biblia.

Labda, baada ya utawala wa miaka -1000, wote watatokea mbele ya kiti cha Mungu cha ukumu, wazuri na wabaya.

Baadhi ya makundi ya kidini wanaamini tu 144,000 wata rithi mbingu. Wenye haki wengine, wanaoamini, wataendelea kuishi milele katika ulimwengu uliotakaswa.

Yuda 1:14-15, *"Na Henoko mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hao, akisema, Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu, maelfu, ili afanye hukumu juu ya watu wote, na kuwaadhibu wote wasiomcha Mungu kwa ajili ya kazi zao zote za upotevu walizozitenda bila kumcha Mungu na kwa ajili ya maneno magumu yote ambayo hao wenye dhambi wasiomcha Mungu, wameyanena juu yake."*

Wakati Yesu akija atakuja kutoa hukumu **"Juu ya wote"** wakati huo. Hakutakuwa na kutenganishwa kwa watakatifu kutoka katika udhaifu hadi kuchaguliwa kwa miaka saba, alafu kutawala nao kwa miaka 1000 kabla wote hawaja hukumiwa.

Jambo la pili, hiki kinachoitwa "kuchaguliwa" inakuwepo tu sehemu ya binadamu akimuangalia Yesu anapokuja.

- Wenye haki wakati atakapoanza uchaguzi.
- Wale wanaoishi duniani baada ya miaka 7 ya uchaguzi.
- Na wale wasio na haki waliokufa ambao wanapaswa kusubiri tena miaka 1000 kabla hawaja muona Kristo.

Ni tofauti wa moja kwa moja na biblia, ambayo inasema:

Ufu. 1:7, *"Tazama yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma; na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake. Naam. Amina."*

Mataifa yote yatakuwepo wakati wa kuja kwake Kristo.

Hiyo iko wazi, kauli yenye mamlaka: "*tazama anakuja na mawingu; na kila jicho litamwona...."*

Mat. 25:31-46 inaeleza kuwa mataifa yote watakuwa mbele ya Kristo wakati wa kuja kwake. Wote wabaya na wazuri watakuwa pale — wote kwa wakati mmoja.

Kutakuwa na safari moja- kuja kwa Bwana mara moja – na hukumu mmoja, wakati ambapo kutakuwa na wakati mgumu wa kutenganisha walio okoka na ambao hawaja okoka.

Hakuna nafasi katika Mat. 25 kwa ajili ya nadharia hii ya wakati wa kuchaguliwa kwa wachache au kipindi cha miaka 1000. Ni nadharia ya uongo iliyoenezwa na Hal Lindsey, aliyeandika kitabu kilichojiuza sana katika mwaka wa 1973, kilichoitwa "Dunia kuu ya Mwisho" ambapo alidai kwamba vita hivi karibia vipo juu yetu.

Mtume Paulo alitoa ufafanuzi ambayo inatupilia mbali hii nadharia ya kuchaguliwa kwa wachache na miaka elfu moja.

2 Tim. 4: 1, *"Nakuagiza mbele za Mungu na mbele za Kristo Yesu, takayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake.*

- Hao walio hai watakuwa pale.
- Hao waliokufa nao watakuwa pale.
- kulingana tulivyo soma, wote wenye haki na wasio na haki watakuwepo.

Nadharia ya kuchukuliwa wachache baada ya miaka elfu moja inasema wenye haki waliokufa hawata tokea kwa miaka mingine 1000. Nadharia hii inapingana kabisa na 2 Tim. 4:1 na mafundisho mengine ya Biblia.

Sababu ya tatu ambayo inaonyesha kuwa nadharia hii ni uongo. Kwa kweli NI kwamba inapinga mafundisho ya wazi ya Biblia:

Yoh. 5:28-29, *"Msisistabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini watasikia sauti yake. Nao watatoka wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu."*

Yesu alisema wenye haki waliokufa na wasiona haki waliokufa, pamoja na hao walio hai watakuja wote kumpokea Bwana wakati mmoja.

Lakini hawa wanaodai kuchukuliwa wachache wanadai kwamba ni wenye haki tu watampokea Bwana wakati wa kuanza kwa uchaguzi huo. Miaka saba baadaye, baadhi tena wanamuona Bwana; alafu baadaye tena miaka 1000 kabla ya wasio na haki kumlaki Bwana.

Biblia inaangamiza nadharia hii ya kuchaguliwa wachache na miaka elfu moja.

Yoh. 5:28-29, *"Msistajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu."*

Yesu akija tena kila jicho hapa duniani lita mwona akiwa mawinguni.

Ufu. 1:7, *"Tazama yuaja na mawingu, na kila jicho lita mwona , na hao waliomchoma, na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake. Naam. Amina."*

Yesu akija tena haji kuanzisha ufalme wake duniani kwa miaka elfu.

1 Wakor. 15:24, *"Hapo ndipo mwisho, atakapompa Mungu Baba ufalme wake na mamlaka yote, na nguvu."*

Yesu aliongelea kurudi kwake itakuwa mara moja- katika siku moja – na vyote kwa wakati mmoja.

- Yoh. 6: 39–44, *"Na mapenzi yake aliyenipeleka ni haya; ya kwamba katika wote alionipa nisipoteze hata mmoja, bali nimfufue siku ya mwisho. Kwa kuwa mapenzi yake Baba yangu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho. Basi Wayahudi wakamnung'unikia, kwa sababu alisema, Mimi ni chakula kilichoshuka kutoka mbinguni. Wakasema Je! Huyu ndiye Yesu, Mwana wa Yusufu ambaye twamjua babaye na mamaye? Sasa asemaje huyu, Nimeshuka kutoka mbinguni? Basi Yesu akajibu akawaambia, Msinung'unike ninyi kw anyi. Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa an Baba aliyenipeleka; name nitamfufua siku ya mwisho."*
- Yoh. 6:54, *"Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; name nitamfufua siku ya mwisho."*
- Yoh. 11:24, *"Martha akamwambia, najua ya kuwa atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho."*

- Yoh. 12:48, *"Yeye anikataaye mimi asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho."*
- Yoh. 5:28-29, *"Msistajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataisikia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu."*

Nadharia hii inapingana na ukweli wa Mungu wa milele, kama inavyofafanuliwa na mtume aliyevuviwa.

2 Wathess. 1:6-10, *"Kwa kuwa ni haki mbele za Mungu kuwa lipa mateso hao wawatesao ninyi; na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake. Katika mwali wa moto huku akiwalipiza kisasi wao wasio mjua Mungu, na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake; yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu wake, na kuustajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile, (kwa sababu ushuhuda wetu ulisadikiwa kwenu."*

Pia ipo katika pingamizi na mtume aliyevuviwa Petro.

2 Pet. 3:10-14, *"Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu na viumbe vya asili vitaunguzwa na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea. Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa, mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza, ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua, na viumbe vya asili vitateketea na kuyeyuka? Lakini kama ilivyo ahadi yake, mnatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake. Kwa hiyo wapenzi kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake."*

Nadharia hii inakataa kitakachotokea "siku hiyo".

Nadharia hii inadai mwendelezo wa dunia kwa miaka saba, tofauti na kuja kwa Bwana.

Na wanaodai miaka elfu wanadai mwendelezo wa dunia kwa miaka 1000 kabla haijachomwa.

Bwana wetu ameweka wazi kwamba yote yatatendeka kwa siku moja. Sisi ni wakina nani tuamini?

Waeb. 9:27, *"Na kama vile watu wanavyowekewa kufa maramoja, na baada ya kufa hukumu."*

Je ukotayari kwa siku hiyo?

Hitimisho

Uko tayari kwa kuja kwake Kristo mara ya pili? Biblia inasema unatakiwa kuwa tayari. Yafuatayo yaonyesha jinsi unaweza kufanya hiyo iwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao."*

  Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja mwenye umri sawa na wa kwangu, aliniambia kwamba haamini kwamba Mungu yupo. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba kuna Mungu. Lakini ili uwe sehemu salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbelel za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda mungu akiona kwamba amekwenda kanisani na kuishi maisha mazuri Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo jehanamu (kama kuna jehanamu). Nikamwambia "haifanyi kazi kwa mfumo huo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza."

- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Matend 11:18, "...Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima</u>."* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu

amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **kuKiri.** Waru. 10: 9 -10, *"Kwama ukimkiri Yesu kwa kinywa chako, na kuaminikwa moyo wako kwamba Mungu alimfufu katika wafu utaokoka. Maana kwa moyo mtu uamini ata kupat haki; na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."* Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

  Angalia hiyo katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamaanisha kuelekea katika kitu Fulani, si kwamba mtu tayari ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubati ambapo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kutimiza haki yote. "*Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zika mfunukia; akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa wangu ninayependezwa naye."* (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu chema kufanya. Unaona jinsi gani Mungu alipendezwa Yohana alipombatiza? Yesu pia akasema *"imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yote, si kwa sababu ni haki yetu.

  Kwa kweli, kama hatuja batizwa bado tupo kwenye dhambi zetu. *"Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matendo. 2:38). Petro, ulisema nini kusudi la ubatizo? "Kwa ajili ya ondoleo la dhambi." Kwa nini yeyote aache hatua hii inayotuondoa dhambi zetu?

  Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu ni lazima tubatizwe.

  *"Akawambia enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminie **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16)

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kile kile, *"Unakawilia nini? Simam, ukabatizwe; na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend 22:16).

Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko.

"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyo unganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena." (Warumi 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu kwa kutumiwa kwa damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tuko huru na dhambi zetu za zamani tunapobatizwa.

Hii haimaanishi kuwa "kunyunyiziwa maji.". Andiko hilo hapo juu inasema ubatizo ni maziko. Mwili uliokufa hatuupeleki makaburini ili linyunyiziwe udongo mdogo juu yake; bali tunauzika mwili.

Kama haujajiandaa kwa ajili ya kuja kwake mara ya pili, kwa nini usizingatie sasa.